



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

MWALIKO WA WATAZAMAJI WA UCHAGUZI MDOGO WA UDIWANI
KATIKA KATA MBILI (02) KWENYE HALMASHAURI ZA MEATU NA
KIBONDO

Kwa mujibu wa kifungu cha 13 (3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuendesha Uchaguzi Mdogo wa Udiwani katika Kata ya **Mwanahina** Halmashauri ya **Meatu** na Kata ya **Biturana** Halmashauri ya Wilaya ya **Kibondo** kujaza nafasi wazi kwenye Kata hizo kutokana kujiuzulu uanachama.

Kwa ajili ya kuweka uwazi katika Uchaguzi huo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia Kanuni ya 14 (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2015, inapenda kualika Asasi za Kiraia na Taasisi mbalimbali za ndani zinazotaka kuwa Watazamaji wa Uchaguzi katika Uchaguzi Mdogo unaotarajiwa kufanyika tarehe **19/01/2019**.

Ratiba ya Uchaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

Na.	Tukio	Tarehe
1.	Kutoa Fomu za Uteuzi	21 - 27 Disemba, 2018
2.	Siku ya Uteuzi wa Wagombea	27 Disemba, 2018
3.	Kampeni za Uchaguzi	28 Disemba, 2018 hadi 18 Januari, 2019
4.	Siku ya Kupiga Kura	19 Januari, 2019

Kata zenye Uchaguzi;

NA	MKOA	NA	HALMASHAURI	NA	KATA
1.	KIGOMA	1.	Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo	1.	Biturana
2.	SIMIYU	2.	Halmashauri ya Wilaya ya Meatu	2.	Mwanahina

Asasi/Taasisi zinapaswa kuzingatia masharti yafuatayo wakati wa kuwasilisha maombi yao:-

- (i) Anuani Kamili ya Taasisi husika,
- (ii) Anuani ya Makazi ya Ofisi ya Taasisi husika ilipo,
- (iii) Mahali /Sehemu ambapo Taasisi husika inafanya kazi.
- (iv) Shughuli ambazo zinafanywa na Taasisi husika kwa mujibu wa Hati ya Usajili
- (v) Kutaja sehemu ambazo Asasi/Taasisi inataka kufanya zoezi hilo la Utazamaji.
- (vi) Kutaja idadi ya watu ambao Taasisi / Asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na taarifa zao.
- (vii) Kutaja majina na namba za simu za viongozi wa Taasisi husika kama yalivyoandikwa katika Hati za Usajili wa Taasisi.
- (viii) Ikiwa Taasisi inahusisha Watendaji wa Kimataifa wawili lazima wawe watanzania.
- (ix) Kuambatanisha nakala/kivuli cha hati ya Usajili wa Taasisi husika.
- (x) Kuambatanisha nakala / kivuli cha Katiba ya Taasisi / Asasi husika.

Vilevile, Taasisi zitakazopewa vibali vya kuwa Watazamaji zitapaswa kuzingatia Mwongozo kwa watazamaji wa ndani na wa Kimataifa ulioandaliwa na Tume kwa mujibu wa Kanuni ya 20 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2015.

Maombi ya kuwa Watazamaji wa Uchaguzi yatapaswa kuwasilishwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Makao Makuu kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Uchaguzi,
Tume ya Taifa ya Uchaguzi,
Posta House, Ghorofa ya 7,
Mtaa wa Ghana/Ohio,
S. L. P. 10923,

DAR ES SALAAM.

Maombi yatatakiwa kuwasilishwa si zaidi ya tarehe 26 Desemba, 2018.